**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ULINZI NA USALAMA WA MTOTO H/W YA MUFINDI KWA KIKAO MAALUM CHA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 06/04/2017**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

katika kikao hiki cha leo tutajikita katika maeneo makuu 4;

Mosi; Kuonyesha takwimu za matukio ya ukatili dhidi ya watoto.
Pili, kutoa ufafanuzi wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto
Tatu, tutaonyesha changamoto kadhaa ambazo hazitakuwa ngeni kwenu labda kwa wajumbe wachache wa baraza hili ambao hawakuwepo tangu tuanze mpango huu kwani kila mwaka sisi tumekuwa na fursa ya kukaa na ninyi hapa kwa agenda hii

Nne na mwisho, tutakaa kimya kupata michango, matamko, maagizo na maazimio ya baraza lako juu ya suala hili la ulinzi na usalama wa mtoto tutakalokuwa tumeliwasilisha.

**Takwimu juu ya Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto**
***Mheshimiwa Mwenyekiti,***

Kumekuwa na matukio mbalimbali ya ukatili toka tuanze mpango huu wa ulinzi na usalama wa mtoto Mwezi Novemba 2013 hadi Marchi 2017.
Mwaka 2013 na 2014 kulikuwa na matukio 168 yaliyoripotiwa kwenye ofisi zetu yakiwemo ya ubakaji 57, ya ubakaji na mimba 8 ya kulawiti -5. Matukio mengine yalikuwa ya watoto kupotea na kuokotwa, kutelekezwa, kupigwa na kuchomwa moto katika miili yao.

Mwaka 2015 kulikuwa na matukio 132 yaliyotolewa taarifa kwenye ofisi zetu. Katika matukio ya mwaka huo wa fedha; matukio 26 yalikuwa ya ubakaji na 6 yalikuwa ya ubakaji na mimba wakati Matukio 2 yalikuwa ya ulawiti. Mwaka 2016 kumeripotiwa matukio 74 ya ukatili, na katika matukio hayo; ni matukio 25 yaliyokuwa ya ubakaji na matukio 6 yalikuwa ya ubakaji na mimba wakati matukio 2 yalikuwa ya kulawiti. Lakini katika kipindi hiki cha karibu miaka 3 yaani 2013, 2014 na hadi Agosti 2015 hakukuwa na hukumu yeyote dhidi ya vitendo hivi iliyotolewa. Na kwa kipindi cha miezi 3 ya Januari, Februari na Machi 2017 tayari kuna matukio ya ukatili 53 ya ubakaji 18, ubakaji na mimba 7 na kulawiti 2. Hii inafanya matukio ya ubakaji tokea 2013 hadi machi 2017 yawe 153.

Mwezi wa 9 mwaka 2015 , timu yetu ilifanya kikao na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya na baadae kikao cha ndani kati ya maafisa ustawi, uongozi wa jeshi la polisi wilaya na mahakama ambapo tuliweka mikakati kufanikisha kesi za matukio ya ukatili.
Baada ya kikao hicho, yaani Kuanzia Septemba 2015 hadi Machi 2017 jumla ya mashauri 36 ya watoto yametolewa hukumu ambapo matukio 32 tulishinda kesi. Jumla ya watuhumiwa 14 Wamehukumiwa vifungo vya miaka 30 kila mmoja, na mtuhumiwa 1 amehukumiwa kifungo cha miaka 60 jela wakati watuhumiwa 2 wamehukumiwa kifungo cha maisha jela kwa makosa ya kulawiti watoto na watuhumiwa 12 Wamehukumiwa vifungo vya nje wakati watuhumiwa 3 Wamehukumiwa kwenda shule ya maadilisho Mbeya.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**
Katika kuhitimisha sehemu hii ya kwanza, Ni kweli kuwa taarifa ya hapo juu inatupatia faraja kwa kutoka matukio 15 kwa mwaka yaliyotolewa taarifa kabla ya mpango huu hadi matukio 68,120,132,84 na 49 kwa miezi 3 tu ya mwaka 2017. Hii inatupatia

faraja kuwa kazi ya kujenga uelewa na kuihamasisha jamii imefanyika na watu wamehamasika kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto.
Lakini pia kutoka hukumu 0 mwaka 2013 – Julai 2015 hadi hukumu 32 kwa sasa si jambo dogo ingawa kwa idadi ya matukio ukilinganisha na hukumu unaweza kufuta kauli ya hapo juu. Hii inatokana na changamoto tutakazoziona kwenye sehemu ya tatu ya taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI; UFAFANUZI WA BAADHI YA MATUKIO YA UKATILI

***Mheshimiwa Mwenyekiti,***

Nifafanue baadhi ya matukio ambayo yanawapata watoto wetu, yapo mengi ambayo ni pamoja na Kupigwa, kuchomwa moto, kuumizwa kihisia, kunyimwa haki mbalimbali ikiwa ni pamoja na elimu, kushikwa maeneo ya utu wao ikiwemo kwenye matako, maziwa na hata mapaja. Haya yote ndiyo yanayojenga masikitiko yetu juu ya watoto hawa

Lakini leo nitafafanua ukatili wa kingono zaidi ambao kwa sasa ni tishio katika halmashauri yetu hasa **ubakaji na ulawiti**
Watoto wetu kwa sasa wako katika janga kubwa la kutendewa ukatili wakiwa majumbani, mashuleni na hata kwenye michezo yao ya kawaida na kwa masikitiko makubwa wanaotenda matukio haya wamekuwa ni wazazi, ndugu, walezi, walimu, na pia watoto wakubwa kuwatendea watoto wenzao wenzao wadogo. Matukio haya mwanzoni timu yetu ilipotoa taarifa kwenye baraza lako ilionekana ni baadhi ya kata ndizo zilizokuwa na matukio hayo lakini kwa sasa ukatili huu unazidi kushika kasi hadi kufika kwenye takribani kata zote.

Naomba kutoa taarifa juu ya baadhi tu ya matukio kwenye orodha kubwa ya matukio yaliyotolewa taarifa ofisini kwetu;

***Imeondolewa kwa maslahi ya mtoto na maadili ya kimahakama kwani kesi nyingi bado zinaendelea mahakamani***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Tunapowasilisha namna hii inaweza kuchukuliwa kuwa ni jambo ambalo tayari limetokea, na kwa kuwa ni mengi yanaanza kuzoeleka kwenye masikio ya watu lakini ni wajibu wetu kuyatafakari kwa kina na kwa ukaribu Zaidi ili kupata hisia ya ikiwa au ingekuwa mwanao, mjukuu wako, au mtoto wa ndugu yako kuwa amebakwa na au kulawitiwa au kupewa ujauzito au kuambukizwa VVU. Tujaribu kufikiri tena, tufikiri kwa undani kwa kuangalia dhamana tulizokabidhiwa za kuwa wawakilishi na watoa maamuzi juu ya mstakabali wa maisha ya watoto hawa ambao kwao sasa hivi dunia ni jehanamu. Na kwamba pengine tukiamua kwa pamoja na kwa dhati tunaweza kuwanusuru ambao wangebakwa au kulawitiwa kuanzia kesho.

**Mheshimiwa mwenyekiti**, inatia huruma na masikitiko makubwa unapobahatika kuwaona watoto wenyewe waliotendewa vitendo hivi, hali wanayokuwa nayo na namna wazazi wao wanaovyoharibu rasilimali kubwa kuwaokoa watoto wao dhidi ya madhara ya vitendo hivi. Wazazi wengine wanaumia Zaidi kwa sababu kunakuwa hakuna tena mustakabari mzuri wa maisha ya watoto wao hasa pale wanapobakwa na kupewa ujauzito kwani ndoto zao hukoma kabisa. Nitoe mifano ya watoto wa malangali, Mninga, Nyololo na Itona

**SEHEMU YA TATU: CHANGAMOTO**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, zipo changamoto ambazo ni kikwazo katika kuifikia Mufindi tunayoitaka itakayoishi na watoto wakawa salama

- Jamii kutokuwa na elimu ya Malezi dhidi ya watoto jambo ambalo kwa sehemu kubwa linachangia watato kufanyiwa ukatili au wale wakubwa kuwafanyia wadogo. Hapa lazima tukubali kuwekeza ili jamii nzima ya watoto na watu wazima wapate elimu hii kwa njia ya mikutano, semina, vikao, vyombo vya habari na vipeperushi. Kuwafikia watoto mashuleni na hata kwenye taasisi mbalimbali wanazoishi. Wazazi lazima watambue kuwa suala siyo kumzaa na kuhakikisha ana kula bali anapaswa kulindwa na kuwekeza kwenye akili yake juu ya nini afanye, nini asifanye, kikitokea kitu tofauti afanye nini. Mfano wa Mninga na Igowole
- Jamii ielewe uthamani wa mtoto, ichukie ukatili dhidi ya watoto na kwamba wachukue hatua stahiki pale panapokuwa na dalili za mtu, watu kutaka kufanya ukatili. Hii iwe ni dhamira ya kila mwanajamii. Mfano kijiji cha Lwing'ulo, Nyololo shuleni.

- Ukosefu wa usafiri stahiki kwa kitengo cha ustawi wa jamii. Kesi nyingi zinashindwa mahakamani kwa kupoteza ushahidi ambao sisi kama kitengo husika tunashindwa kabisa kuzifanyia uchunguzi wa kina ili kuziwasilisha mahakamani. Jambo hili la usafiri lina athari hata kwa watoto moja kwa moja pale tunaposhindwa kuwafikia ili wapate huduma sahihi kwa wakati.Tunapigiwa simu kila mara kutoka sehemu tofauti tofauti ambapo kimsingi tunashindwa kuwafikia wahusika na

hii inawakatisha tamaa hata wanaotupatia taarifa toka kwenye jamii. Ofisi yetu ilipaswa kuwa na usafiri ambao hata dereva wake anawezeshwa na kukubali kuwa analo gari la dharura. Usafiri umekuwa pia kikwazo cha kufanya kazi ambazo wafadhili wameshatuwezesha au kuzifanya baada ya miezi kadhaa tokea ziwe tayari.Hapa kuna changamoto ambayo hata kiukaguzi wa fedha inatuletea sintofahamu na watumishi wa ukaguzi wa ndani na hata wa nje wanapokuja. Katika hili nizishukuru sana ofisi za mkaguzi wa ndani na mipango vinginevyo hali ingekuwa tete zaidi

- Uchache wa maafisa ustawi wa jamii jambo ambalo kwa sehemu kubwa linafanya utekelezaji wa kazi kuwa mgumu Zaidi au kufanya kazi kwa kujitesa jambo ambalo linaweza kuondoa au kupoteza ufanisi wa kazi kwa maafisa husika.
- Ufinyu wa bajeti ya mapato ya ndani kwa kitengo cha ustawi wa jamii jambo ambalo pamoja na mapato kuwa madogo lakini pia kutopewa kipaumbele katika Nyanja mbalimbali. Hii inaathiri hata jitihada za wafadhili
- Kutokuwekwa mkakati wa makusudi na wa lazima kunusuru majanga kwa watoto ikiwemo ngazi za kitongoji, kijiji, kata na kwenye halmashauri hivyo jambo hili kubakia la watu wachache au ofisi moja tu
- Wingi wa matukio unaohitaji utayari na uharaka ukilinganisha na uwepo wa rasilimali. Kitengo cha ustawi wa jamii kwa upande wake kinahusika na makundi maalumu jambo ambalo wateja wake kila mara ni wale ambao huwezi fikiria kuwahudumia kesho wala wiki inayokuja.
- Kutokuwepo kwa fedha za dharura za kutoa huduma kwa watoto wanaohitaji huduma za haraka na za lazima n ahata zikiwepo pia zinakutana na changamoto za matumizi ya fedha za serikali. Tunalazimika wakati mwingine kujitoa kunakoathiri

utumishi wetu, mathalani Igomaa, watoto wawili wa Mbalamaziwa,

**Mheshimiwa mwenyekiti**, kuna changamoto nyingine lakini nikiri kuwa kubwa ni hizo ambazo zimekuwa kikwazo kwa ufanisi wa jambo hili. Mapendekezo yetu ni kuona kuwa kila mwanajamii anakuwa sehemu ya vita hii na anakuwa tayari kujitoa kwa maslahi ya mtoto. Wapo watu ambao wamewahi kutumia magari yao binafsi toka kwenye kata zao kuwaleta watoto mjini

## SEHEMU YA NNE; KUPOKEA USHAURI NA MAAZIMIO

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kikao cha 4 kwa baraza lako kupokea taarifa za aina hii na kuomba usaidizi juu ya kukabiliana na janga hili. Kila mwaka tunapokutana vitendo hivi vimekuwa vikizidi kuongezeka kwa kasi na siyo kupungua. Na kila mara tumekuwa tukiandika taarifa juu ya matokeo ya vikao hivi ili kuwajuza wafadhili yaliyojadiliwa. Niombe sasa kuwasilisha na kuwa tayari kupokea ushauri juu ya utatuzi wa changamoto hizi.

**NAOMBA KUWASILISHA**

**Imeandaliwa na**
**Nyamara Elisha**
**Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)**
**Mufindi.**